## HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO

## TAARIFA YA MGAWANYO WA FEDHA ZA LGDG KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 1.0 UTANGULIZI

Fedha za LGDG ni fedha ambazo zinatoka serikali kuu kwa ajili ya kusaidia nguvu za wananchi katika miradi ya Vijiji, kama ilivyo kwa Wilaya zingine za Tanzania bara Wilaya ya Gairo pia imepata fedha hizo za LGDG kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

### 2.0 MAPOKEZI YA FEDHA ZA LGDG

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 H/Wilaya ya Gairo iliweka katika Bajeti yake kiasi cha Tshs 627,436,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji ya miradi mbalimbali iliyopo katika Wilaya, ambapo mpaka tarehe 30 Juni 2017 Halmashauri ilipokea kiasi cha Tshs 242,915,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.Kiasi cha Tshs 121,626,000.00 kimepokelewa tarehe 02.12.2016 na kiasi cha Tshs 121,289,000.00 kimepokelewa na tarehe 12.01.2017 kwa ajili ya kusaidia miradi viporo.Miradi iliyotekelezwa na fedha za CDG kama inavyoonekana hapa chini.

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA CDG KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### MIRADI YA SEKTA YA AFYA

1) ***Mradi wa Zahanati ya Makuyu***

   Mradi huu ulianza mwaka 2010 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa kijiji cha Makuyu na maeneo ya jirani. Mradi hadi sasa umegharimu ***Tshs 34,355,975.00***. Kati ya fedha hizo, Wananchi wamechangia ***Tshs 10,068,000.00***, Serikali kupitia CDG ya mwaka 2016/2017 imechangia Tshs cha ***Tshs 22,637,975.00*** na Mfuko wa Jimbo mwaka 2011/2012 ulitoa mifuko **100** yenye thamani ya Tshs ***1,650,000.00*** ya simenti.Mpaka sasa ujenzi upo katika hatua ya umaliziaji kwa kipande cha zahanati.



*Zahanati ya Makuyu*

2) ***Mradi wa Zahanati ya Kumbulu***

Mradi huu ulianza mwaka **2004** kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa kijiji cha Kumbulu na maeneo ya jirani. Mradi umegharimu kiasi cha **Tshs 28,409,500.00**,ambapo Wanachi wamechangia **Tshs 12,500,000.00** na serikali imechangia **Tshs 7,784,500.00** (ikiwa **CDG 2012/2013 Tshs 6,680,000 na CDG 2016/2017 Tshs 1,104,500.00)** pia Mh.Mbunge wa Jimbo la Gairo alichangia **bati 63, simenti mifuko 50** na fedha taslimu kiasi cha **Tshs** ***1,000,000.00.*** Mpaka sasa ujenzi umekamilika na huduma zimeanza kutolewa tangu tarehe **11.08.2017.**

3) ***Mradi wa Zahanati ya Ndogomi***

Mradi huu umechangiwa na wananchi pamoja na serikali iliyochangia kiasi cha ***Tshs 1,707,000.00.*** Mpaka sasa ujenzi umekamilika.

### *4) Mradi wa Zahanati ya Meshugi*

Mradi huu ulianza mwaka 2006 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa eneo la Meshugi na maeneo ya jirani. Mradi umegharimu Tshs ***19,151,300.00*** ambapo Wanachi wamechangia Tshs **12,425,300.00**, **CDG 2016/2017** imechangia kiasi cha Tshs ***6,426,000.00.*** GPG 2016/2017 imechangia Tshs ***300,000.00*** fundi anadai kiasi cha Tshs ***2,993,000.00*** Mpaka sasa mradi umekamilika na huduma imeanza kutolewa tangu tarehe **25.07.2017.**



### *5) Mradi wa Kituo cha Afya - Chakwale*

Mradi huu ulianza mwaka 2010 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa kijiji cha Chakwale na maeneo ya jirani. Mradi umegharimu ***Tshs 28,885,763.00*** Kati ya kiasi hicho cha fedha, Wanachi wamechangia ***Tshs 9,516,263.00***, Mfuko wa jimbo umechangia mabati 144 yenye thamani ya ya Tshs ***3,168,000.00*** Wilaya ya mama ya Kilosa ilichangia ***Tshs 8,500,000.00*** na CDG mwaka 2016/2017 imechangia kiasi cha ***Tshs 7,621,500.00.***Mpaka sasa mradi bado unaendelea madirisha yanakamilishwa.

6) ***Mradi wa Zahanati katika Kijiji cha Ibuti***

Mradi huu ulianza mwaka 2007 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa kijiji cha Ibuti na maeneo ya jirani. Mradi umegharimu ***Tshs 48,063,100.00.*** Kati ya kiasi hicho cha fedha, Wanachi wamechangia **Tshs 24,100,000.00** na Serikali kupitia CDG 2016/2017 imechangia kiasi cha ***Tshs 23,963,100.00.***Mpaka sasa mradi upo katika hatua za mwisho za umaliziaji na shimo la choo limechimbwa.



***Zahanati ya Ibuti***

7) ***Mradi wa Zahanati ya Kisitwi***

Mradi huu ulianza mwaka 2007 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi wa kijiji cha Kisitwi na maeneo ya jirani. Mradi umegharimu ***Tshs 36,058,000.00.*** Kati ya kiasi hicho cha fedha, Wanachi wamechangia ***Tshs 15,734,100.00*** , Serikali kupitia CDG 2016/2017 imechangia kiasi cha **Tshs 19,372,500.00** na GPG imechangia kiasi cha ***Tshs 951,500.00.***Pia choo kimegharimu kiasi cha Tshs ***10,397,000.00*** ambapo wananchi wamechangia Tshs ***2,053,000.00,***Mkuu wa Wilaya amechangia mifuko 10 ya simenti yenye thamani ya **Tshs *130,000.00,***Mh Mbunge amechangia bati 12 zenye thamani ya

Tshs ***264,000.00*** na Serikali kupitia GPG imechangia Tshs ***7,950,000.00.***Mpaka sasa mradi umekamilika na huduma zimeanza kutolewa tangu tarehe 25.07.2017



***Zahanati ya Kisitwi***

***MIRADI YA SEKTA YA ELIMU***

***1)Mradi wa madarasa 3 katika Shule ya Msingi Lolela***

Ujenzi wa madarasa 3 na Ofisi katka shule ya Msingi Lolela ulianza mwaka 2014. Lengo la mradi ni kuanzisha shule rasmi baadala ya kuendelea kuwa Mkondo wa shule ya Msingi.Mpaka sasa mradi umegharimu kiasi cha Tshs ***37,971,550.00*** *ambapo* Michango ya wananchi ***Tshs 8,599,350.00*** na serikali kuu kupitia CDG 2016/2017 imechangia kiasi cha *Tshs* ***29,372,200.00***. Mpaka sasa mradi huu umekamilika na madarasa yameanza kutumika tangu tarehe **28.07.2017.**



***Shule ya Msingi Lolela***

***2)Mradi wa madarasa 2 katika S/Msingi – Gairo B***

Mradi huu ulianza mwaka 2017 kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule ya Msingi Gairo B .Mradi umegharimu kiasi cha ***Tshs 21,089,500.00*** ambapo wananchi wamechangia kiasi cha .***Tshs 6,500,000.00*** na serikali kupitia CDG 2016/2017 imechangia ***Tshs 14,589,500.00*** .Mpaka sasa ujenzi umekamilika na umeanza kutumika tangu tarehe **28.07.2017.**



***Shule  ya Msingi Gairo B***

***3) Mradi wa madarasa 2 katika Shule ya Msingi Mnjilili***

Mradi huu ulianza mwaka 2006 kwa lengo la kupunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi katika S/Msingi Mnjilili.Mradi umegharimu kiasi cha Tshs ***16,842,000.00*** ambapo Wanachi wamechangia Tshs ***3,500,000.00*** na CDG 2016/2017 imechangia Ths ***6,523,000.*****00** pia mfuko Jimbo mwaka 2011/2012 umechangia mabati 99 yenye thamani ya Tshs ***2,526,500.00*** na Mfuko wa Jimbo mwaka 2013/2014 umechangia kiasi cha Tshs **4,292,500.00**.Mpaka sasa mradi umekamilika na umeanza kutumika tangu tarehe **28.07.2017.**



***Shule ya Msingi Mnjilili***

***4)Mradi wa madarasa 2 katika S/Msingi Makuyu***

Mradi huu ulianza mwaka 2004 kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule ya Msingi Makuyu.Mradi huu umegharimu kiasi cha Tshs ***14,324,125.00*** ambapo wananchi wamechangia Tshs ***8,500,000*.00** , Serikali imechangia mbao 150 kutoka mfuko wa jimbo zenye thamani ya Tshs ***1,050,000.00***, pia CDG 2016/2017 imechangia ***Tshs 4,774,125.00.*** Mpaka sasa ujenzi umekamilika na jengo limeanza kutumika

***5)Mradi wa madarasa katika Sekondari ya Majembwe***

Mradi huu ulianza mwaka 2017 kwa lengo la kupunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi katika S/Sekondari ya Majembwe .Mradi umegharimu Tshs ***20,802,100.00*** ambapo Wananchi wamechangia Tshs ***5,786,000.00*** na Serikali kupitia CDG 2016/2017 imechangia *Tshs* ***15,116,100.00***.Mradi umekamilika na umeanza kutumika tangu tarehe **28.07.2017.**



***Shule ya Sekondari Majembwe***

***6)Mradi wa Chumba Kimoja cha maabara katika Shule ya Sekondari ya Chanjale***

Mradi ulianza mnamo mwaka 2014 kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi ili waweze kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.Mradi umegharimu kiasi cha Tshs **27,189,700.00,** wananchi wamechangia Tshs **9,558,700.00,** CDG mwaka 2016/217 imechangia Tshs ***16,433,000.00***, na GPG 2016/2017 imechangia kiasi cha Tshs ***1,198,000.00*** .Mpaka sasa mradi umekamilika.



***Maabara Sekondari ya Chanjale***

***7)Mradi wa maabara 1 katika Shule ya Sekondari Kibedya***

Mradi huu ulianza mwaka 2014 kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi ili waweze kujifunza kwa vitendo .Mradi umegharimu kiasi cha Tshs **22,846,283** ,ambapo wananchi wamechangia ***Tshs 6,409,333.00*** CDG 2014/2015 ***Tshs 6,665,000 .00***, na CDG 2016/2017 ***Tshs 9,771,950.00*** Mpaka sasa kazi ya ujenzi bado inaendelea

***8)Ujenzi wa Maabara katika S/Sekondari Chagongwe***

Mradi ulianza mwaka 2014 kwa lengo kuwasaidia wanafuzi wa sekondari ili waweze kujifunza kwa vitendo. Mradi umegharimu kiasi cha ***Tshs 46,437,200.00*** ambapo wananchi wamechangia Tshs ***15,569,200.00*** CDG 2014/2015 imechangia Tshs **6,265,000.00** na wadau wamechangia mifuko 40 ya simenti yenye thamani ya Tshs **600,000.00 CDG 2016/2017** imechangia ***Tshs 24,003,000.00*** .Mpaka sasa Ujenzi bado unaendelea.

**10*)Mradi wa nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Tabu-Hotel***

Mradi huu umechangiwa na wananchi pamoja na serikali,kwa lengo la kuwasaidia walimu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi .Serikali kupitia CDG 2016/2017 imechangia ***Tshs 12,443,230.00.*** mpaka sasa mradi huu bado unaendelea na ujenzi

*9)Mradi wa matundu ya vyoo katika S/Msingi Gairo A*

Mradi huu ulianza mnamo mwaka 2016 kwa lengo la kupunguza tatizo la choo katika shule ya Msingi Gairo.Mradi umegharimu kiasi cha Tshs ***8,760,000.00*** ambapo wananchi wamechangia kiasi cha Tshs ***5,300,000.00*** na CDG mwaka 2016/2017 imechangia kiasi cha Tshs ***3,460,000.00*** Mpaka sasa mradi bado unaendelea.



***Shule ya Msingi Gairo A***

.